

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAISI  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SIMU YA UPEPO: “REGCOM “  
SIMU NA:- 023-220-2098  
FAX NA. 023-220-2502  
Email: [ras.lindi@pmoralg.go.tz](mailto:ras.lindi@pmoralg.go.tz)



OFISI YA MKUU WA MKOA,  
S.L.P. 1054,  
LINDI.  
26, Mei 2018

**TARATIBU ZA USAJILI WA KAMPUNI ZA UNUNUZI WA ZAO LA  
UFUTA MSIMU 2017/2018**

Mkoa unawatangazia wanunuzi wote wa zao la ufuta kuwa, Msimu wa ununuzi wa zao la ufuta utanza rasmi tarehe 01/06/2018. Mfumo wa ununuzi utakaotumika ni ukusanyaji wa ufuta kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi na kuuzwa kupitia minada itakanyofanyika kila siku ya jumanne na Jumatano ya wiki katika maeneo yanayolima zao hili.

Wanunuzi wote wanatakiwa kujisajili Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi kabla ya kwenda kushiriki katika minada itakayofanyika. **(Hakuna kampuni itakayoruhusiwa kushiriki bila kusajiliwa).**

Mambo muhimu yatakayohitajika ili kampuni iweze kusajiliwa ni:-

- i. Nakala ya leseni hai ya biashara (valid business license).
- ii. Nakala ya cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN/VAT Certificate).
- iii. Nakala ya hati ya kutodaiwa kodi ya ndani ya nchi (Tax clearance)
- iv. Nakala ya cheti cha usajili wa kampuni (Certificate of incorporation/certificate of registration).
- v. Picha mbili za rangi za wakurugenzi wa kampuni
- vi. Taarifa za benki zisizopungua miezi mitatu (Bank statements).
- vii. Kujaza fomua na.1

Imeandaliwa na:-

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa  
S.L.P 1054  
**LINDI.**